

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI**

**24 MEI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI – TAREHE 24 MEI, 2023**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

## **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

#### **415. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali imefikia wapi kuhusu Mchakato wa Pansheni kwa Wazee wote.

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **416. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini barabara ya Majengo, Ruvuma, Subira na Muungano itajengwa kwa kiwango cha lami.

**417. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga miundombinu ya maji shuleni ili kuepusha milipuko ya magonjwa.

**418. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini mradi wa ujenzi wa Soko la kisasa Tengeru utatekelezwa ili kuongeza mapato na kuboresha huduma kwa Wananchi.

**419. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kuweka utaratibu kwa Wananchi kuwasilisha Hoja Binafsi mbele ya Mabaraza ya Madiwani.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**420. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUWAKALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, zimebaki changamoto ngapi za Muungano kutatuliwa baada ya kufanyika jitihada za kuzipunguza.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**421. MHESHIMIWA DAVID MWAKIPOSA KIHENZILE (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itakamilisha usajili wa *International Federation of Red Cross and Crescent* nchini.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **422. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini fedha itatengwa kufanya usanifu na upembuzi yakinifu wa Mradi wa kutoa maji Ziwa Nyasa kupeleka Tarafa ya Masasi - Ludewa.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **423. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Mwembe – Mbaga hadi Mamba kwa kiwango cha lami.

### **424. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga angalau kilometa tano kwa kiwango cha lami Barabara ya Tunduru - Mtwara Pachani.

**425. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Utekelezaji wa Mradi wa Mtwara *Corridor* umefikia hatua gani.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**426. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, nini mpango wa Serikali kuingiza lugha ya alama kwenye Mitaala ya Elimu nchini.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

**427. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, kuna mpango gani wa kutoa mwongozo kwa Wawekezaji kuchangia shughuli za maendeleo katika maeneo wanayowekeza.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **428. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mpango gani wa kupeleka mbegu za mahindi kabla ya kipindi cha masika katika Jimbo la Mbulu Vijijini.

## **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

### **WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA  
24 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**